## 1 (LAZIMA)

### **USHAIRI**

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

#### WASAKATONGE

# 1. Wasakatonge na juakali

Wabeba zege ya maroshani, Ni msukuma mikokoteni, Pia makuli bandarini, Ni wachimbaji wa migodini, Lakini maisha yao chini.

# 2. Juakali na wasakatonge

Wao ni <u>manamba</u> mashambani, Ni wachapa kazi viwandani, Mayaya na madobi wa nyumbani, Ni matopasi wa majaani, Lakini bado ni masikini.

# 3. Wasakatonge na juakali

Wao huweka serikalini, Wanasiasa madarakani, Dola ikawa mikononi, Wachaguliwa na ikuluni, Lakini wachaguaji duni.

### 4. Juakali na wasakatonge

Wao ni wengi ulimwenguni, Tabaka lisilo ahueni, Siku zote wako matesoni, Ziada ya pato hawaoni, Lakini watakomboka lini? (Mohammed Seif Khatib)

- (a) "Shairi hili ni la kukatisha tamaa". Fafanua rai hii kwa kutoa mifano minne. (alama 4)
- (b) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima na uonyeshe mifano miwili ya jinsi ilivyotumika. (alama 3)
- (c) Eleza umbo la shairi hili.

(alama 5)

(d) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari.

(alama 4)

(e) Onyesha mifano miwili ya maadili yanayojitokeza katika shairi hili.

(alama 2)

^ ^ ^

**TAMTHILIA** Jibu swali la 2 au la 3. Kithaka wa Mberia: Kifo Kisimani 2 Ukitumia mifano, onyesha matumizi matano ya mbinu ya ishara kama ilivyotumiwa katika tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20) 3 "Kwa hakika, kama mzazi hana kifani katika Butangi nzima. Na pengine hata katika ulimwengu mzima." (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4) (b) "Watu waliojiita washauri wa Mtemi Bokono walikuwa si washauri halisi bali wanafiki waliomdanganya." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mitano. (alama 16) RIWAYA Jibu swali la 4 au la 5. Z. Burhani: Mwisho wa Kosa. 4 "Wanawake katika riwaya ya Mwisho wa Kosa wamepewa nafasi ndogo katika masuala ya maendeleo ya kijamii." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano kumi. (alama 20) 5 Eleza jinsi wahusika wafuatao wanavyoafiki anwani ya riwaya ya Mwisho wa Kosa: Ali (a) (alama 10) (b) Asha (alama 10)

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi.

(alama 2)

**(f)** 

(i)

(ii)

Manamba

Tabaka lisilo ahueni

### **HADITHI FUPI**

K. W. Wamitila (mhariri): Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine

6 "Umdhaniaye ndiye, kumbe siye". Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

## **FASIHI SIMULIZI**

7 Fafanua sifa zozote kumi za mtambaji bora wa ngano.

(20 alama)

More Past Paper available on <a href="http://www.kenyaplex.com/questionpapers">http://www.kenyaplex.com/questionpapers</a>